



NTC/L.30/006/119

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NEWALA**



21/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Newala anapenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi ifuatayo:-

MTENDAJI WA MTA A DARAJA LA III – NAFASI (14)

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (cheti) "NTA Level 5" katika fani zifuatazo:-
Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Jamii kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA MTA A

- i. Kuwa Katibu wa Kamati ya Mtaa;
- ii. Mtendaji Mkuu wa Mtaa;
- iii. Mratibu wa utekelezaji wa sera na Sheria zilizotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- iv. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa;
- v. Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa;
- vi. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama;
- vii. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini katika Mtaa;
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- ix. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa; na
- x. Kuwajibika kwa Mtendaji wa Kata

MSHAHARA

Cheo cha Mtendaji wa Mtaa darajala III kina Mshahara wa TGS B kwa mwezi

MASHARTI YA UJUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa

- Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishie barua yake ya maombi kwa Mwajiri wake
- Mwombaji aambatanishe maelezo yake binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu
- Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali
- *Testimonials, Provisional results, Statements of results* n.k hazikubaliki
- Waombaji waweke picha moja ya passport size katika barua zao za maombi
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **03/06/2022** saa tisa alasiri

Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapa chini

Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji Newala
186 Barabara ya Masasi
Mtaa wa Tupendane
S.L.P 39
63482 NEWALA



Shamim D. Mwariko
**MKURUGENZI WA MJI
NEWALA**

NAKALA

- " Katibu
Ofisi ya Rais
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma
S.L.P 2320
DODOMA
- " Tovuti ya Halmashauri
www.newalatc.go.tz
- " Mbao za Matangazo